

## Fomu Fupi ya Kibali cha Kushiriki katika Utafiti

Unaombwa ushiriki katika utafiti. Kabla ya kukubali kujiunga na utafiti, ni muhimu kwamba upokee ufafanuzi wazi wa utafiti kwa lugha unayoelewa. Ifuatayo ni orodha ya yale unayokubaliana nayo unapotia sahihi kwenye fomu hii ya kibali.

Mfasiri ambaye huenda akawa mmoja wa wachunguzi wanaotekeleza utafiti huu au mmoja wa wawakilishi wao amekueleza kuhusu (1) madhumuni ya utafiti huu, utaratibu, na muda ambao utafiti utachukua; (2) utaratibu wowote wa majaribio; (3) hatari yoyote inayoweza kutarajiwa kwa maana, usumbufu na manufaa ya utafiti; (4) uwezekano wa manufaa wa utaratibu au tiba zozote mbadala; na (5) jinsi ya kudumisha usiri.

Ulipoelekezwa kwenye utafiti huu, uliambiwa kuhusu (1) fidia au tiba yoyote ya kiafya inayopatikana kama ukiumia wakati wa utafiti huu; (2) uwezekano wa hatari zisizotarajiwa (hatari zisizojulikana kwa wakati huu); (3) hali ambapo mchunguzi huenda akasimamisha kushiriki kwako; (4) gharama yoyote ya ziada kwako; (5) kitakacho fanyika ukiamua kuwacha kushiriki; (6) wakati gani utaambiwa kuhusu matokeo mapya yanayoweza kuathiri mapendeleo yako ya kushiriki; na (7) idadi ya watu watakaokuwa katika utafiti.

Umeambiwa kwamba kama utajeruiwa kutokana na kushiriki wako katika utafiti huu, utapewa huduma ya afya ya dharura inayohitajika. Hata hivyo, hakuna ahadi ya Chuo Kikuu cha Wayne State na majumui wake ya kukupa fidia ya kifedha au huduma ya kimatibabu ya bure ikiwa utapata jeraha linalohusiana na utafiti huu.

Umeambiwa unaweza kuwasiliana na \_\_\_\_\_, Mchunguzaji Mkuu (the Principal Investigator (PI)) aliye \_\_\_\_\_, kama una maswali kuhusu au matatizo na utafiti huu na uwasiliane na Ofisi ya Utawala wa Bodi ya Ukaguzi ( Institutional Review Board Administration Office) kwa nambari 313-577-1628 kama una maswali yoyote kuhusu haki zako kama mshiriki wa utafiti, utafiti huu, au unachofaa kufanya kama utajeruhiwa.

Umeambiwa kwamba ushiriki wako katika utafiti huu ni wa hiari na kwamba hautaadhibiwa wala hautanyimwa fadhila ikiwa utakataa kushiriki au amua kuwacha kushiriki baada ya kukubali kushiriki.

Kama ukikubali kushiriki, umeambiwa kwamba utapewa nakala ya hati hii iliyotiwa sahihi na mhusari wa maandishi wa utafiti huu wa lugha ya Kiingereza.

Kwa kutia sahihi hati hii kunamaanisha kwamba umeelezewa kwa mdomo juu ya utafiti huu, ikiwa ni pamoja na maelezo yaliyo hapa juu, na kwamba umekubali kushiriki kwa hiari yako.

\_\_\_\_\_  
Sahihi ya Mshiriki/Mwakilishi Aliyeidhinishwa Kisheria/Uhusiano

\_\_\_\_\_  
Tarehe

\_\_\_\_\_  
Sahihi ya Shahidi

\_\_\_\_\_  
Tarehe

\_\_\_\_\_  
Sahihi ya Mfasiri

\_\_\_\_\_  
Tarehe

08/06/03 Toleo #1

08/18/03 Toleo #2

09/17/03 Imeidhinishwa na Kamati ya Utekelezaji